TALKING NOTES ZA MHE. THOBIAS E. M. ANDENGENYE, MKUU WA MKOA WA KIGOMA WAKATI WA KUFUNGUA KIKAO CHA KAMATI YA USHAURI YA MKOA WA KIGOMA

TAREHE 03 DESEMBA, 2021

==========

UTANGULIZI

Mheshimiwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi, Mkoa wa Kigoma,

Ndugu, Katibu Tawala wa Mkoa,

Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya,

Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Kigoma wote mliohudhuria,

Mstahiki Meya wa Manispaa ya Kigoma/Ujiji,

Waheshimiwa Wenyeviti wa Halmashauri,

Wakurugenzi wa Halmashauri,

Waheshimiwa Viongozi wa Vyama vya Siasa mliohudhuria,

Watumishi wa Sekretarieti ya Mkoa wa Kigoma,

Waheshimiwa Wazee maarufu,

Maafisa Watendaji na Waalikwa wote wa Taasisi za Serikali na zisizo za Kiserikali,

Ndugu Wanahabari,

Wageni waalikwa,

Mabibi na Mabwana

Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!

Nianze kwa kumshuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutupa uhai na afya njema hadi tumeweza kukutana katika kikao hiki muhimu chenye lengo la kushauriana, kubadirishana na kupeana dira ya masuala ya maendeleo ya Mkoa wetu.

Niwakaribishe sana wajumbe wote na waalikwa katika kikao hiki, muwe huru kuchangia hoja katika mada na agenda zitakazozungumzwa.

Ukusanyaji wa Kodi na Mapato

Vyanzo vyetu vya mapato tunapaswa kuvipitia upya na kupanua wigo wa ukusanyaji pamoja na usimamizi thabiti katika kukusanya, bado kuna fedha nyingi zinapotea kwa sababu ya usimamizi hafifu kwa wakusanya mapato. Niwakumbushe watendaji katika Halmashauri kuendelea kusimamia kikamilifu Suala ukusanyaji kodi, na kusimamia mifumo ya ukusanyaji kodi kwa njia ya Mashine za Kielektroniki za EFD.

Kutenga maeneo ya viwanda, uwekezaji na machinga

Agizo la Viongozi wetu wa Kitaifa kila Halamshauri kuwa na maeneo kwa ajili ya viwanda, Uwekezaji na Machinga. Katika hali isiyokuwa ya kawaida Mamlaka za Seriakali za Mitaa zimebainisha na kutenga maeneo lakini maeneo haya hayana miundombinu muhimu ambayo inapaswa kuwepo ili kutoa huduma kwa watumiaji. Kupitia Vikao vya Mabaraza tuangalie na kuweka mikakati madhubuti ya kuahkikisha maeneo yanayotenga yanakuwa na miundombinu stahiki.

Uwezeshaji na Biashara

Bado kuna msukumo na dhamira ndogo katika eneo la utengaji na utoaji wa Asilimia kumi kwa makundi ya Vijana, Wenye Ulemavu na Kinamama. Agizo la Serikali la kuwawezesha Vijana, kinamama na Wenyeulemavu kupitia asilimia 10 ya makusanyo ya ndani, Halamsahauri hakikisheni mnatekeleza, maagizo haya ni ya msingi kwa maendeleo ya watu wetu. Kuna vijana na Wananchi wenye ari ya kukuza uchumi nap engine kutengeneza ajira lakini wanakosa fursa kwa kukosa mitaji. Mamlaka za Serikali za Mitaa angalieni namna ya kukopesha makundi hayo ili kutengeneza ajira nyingi kwa wananchi, napengine hii ndiyo njia ya kutengeneza vyanzo vya mapato.

Suala la kilimo na uharibifu wa Mazingira

Namna pekee ya kuwasaidia Wananchi katika Kilimo ni Viongozi na wataalamu kuwapa elimu na uwezesho. Suala la kuendele kulima kwa jembe la Mkoano halina tija tena, Viongozi katika Halmshauri jaribuni kufikiria nje ya boksi kupata Matrekta Kila Wilaya ili wananchi waweze kuyatumia kwa Kilimo chenye tija.

Aidha katika maeneo mengi kilimo cha kuhamhama kimeanza kuharibu mazingira, aidha wananchi kulima kwenye vyanzo vya maji nalo limekuwa tatizo. Viongozi na Watendaji nawakumbusha Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akiwa Jijini mwanza aliagiza Viongozi katika Mikoa yetu na Wilaya tufuatili na kudhibiti uharibifu wa vyanzo vya maji.

Niwakumbushe tu kuwa suala hili linapswa kusimamiwa katika ngazi zote, hivyo tuhakikishe tunasimamia kikamilifu suala la wananchi kuharibu vyanzo vya maji.

Miundombinu ya Elimu na Afya

Serikali imeendelea kuwekeza fedha nyingi sana katika sekta ya Afya ambapo hivi sasa kila Halmashauri kuna miradi mingi ya Elimu na Afya ianendelea kujengwa na mingine ipo katika hatua ya ukamilishwaji. Rai yangu tushirikiane kufuatilia na kusimamia ili miradi hii iweze kukidhi nia njema ya serikali ya Rais wa Jamhuri ya Muuungano wa Tanzania wetu mpendwa mama Samia Suluhu Hassan ambaye ameamua kwa dhati kuhakikisha suala la madarasa na madawati linafikia tamati.

Sensa ya Watu na Makazi

Pili, nchi yetu inatarajia kuwa na zoezi la Sensa Mwaka 2022 kwa mwezi ambao Serikali itatangaza, niwaombe Wananchi wote washiriki katika zoezi la kuhesabiwa ili kuwezesha nchi kutengeneza mipango na Sera zinazoendana na Idadi ya Wananchi waliopo, zoezi la Sensa ni muhimu sana katika maendeleo ya nchi na kwa kila Mwananchi, hivyo wakati ukifika wa kuhesabiwa Wananchi wote watoe ushirikiano kwa wataalamu watakaofika kwenye maeneo kuwahesabu

Uwekaji wa Anuani za Makazi

Nchi yetu pia inatarajia kuweka anuani za makazi katika miji, vitongoji, vijiji katika maeneo yote nchini. Zoezi hili linalenga kurahisisha utambuzi wa makazi ambao ndio ustarabu wa dunia kumtambulisha mtu anapoishi nah ii ni hatua muhimu sana katika suala zima la kimaendleo

Kuendelea kujikinga na UVIKO -19

Aidha, kabla kuhitimisha hotuba yangu naomba niwakumbushe muendelee kuchukua tahadhari ya janga la UVIKO 19 kwa kufuata maelekezo ya Wataalamu wetu wa Afya ikiwemo kuendelea kunawa mikono kwa maji tiririka na sabuni, kuvaa barakoa, kuepuka misongamano isiyo ya lazima na pia Kutumia fursa ya kuchanja kwani kuchanja ni kujiweka salama zaidi ya maambukizi na utakapougua usiwe katika hali tete ya kuwekewa Mitungi ya gesi na kukaa muda mrefu hospitalini.

Waheshimiwa wajumbe na waalikwa,

Viongozi pamoja na Watendaji wote katika Mkoa hatuna budi kuongeza juhudi na ubunifu katika utekelezaji wa shughuli za Umma.

Wakuu wa wilaya na Wakurugenzi hakikisheni migogoro ya Ardhi mnaishughlikia kwa kuzingatia Matumizi bora ya Ardhi, ili kuondoa migogoro kati ya Wakulima na Wafugaji. Kero za wananchi tuzitafutie majawabu yanayotosheleza na kwa wakati. Kila mmoja wetu atimize wajibu wake ipasavyo kwa kutanguliza mbele maslahi ya Umma.

Baada ya kusema hayo, sasa ninayo furaha kutamka rasmi kuwa Kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC) cha pili kwa mwaka 2020/2021 nimekiahirisha rasmi.

Akhsanteni kwa Kunisikiliza.